# JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE

MKATABA WA UWEKEZAJI KATIKA ENEO LA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE

UMETENGENEZWA CHINI YA KIFUNGU CHA 31 (7) CHA SHERIA YA WANYAMAPORI NA.5 YA MWAKA 2009

KATI YA

BODI YA WADHAMINI YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE (JUHIBU)

NA

KAMPUNI YA EBN HUNTING SAFARIS LIMITED TANZANIA


IMETAYARISHWA NA:

JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE,

S.L.P. 104, BABATI-MANYARA

E-mail: burungewma@gmail.com

**MKATABA WA UWEKEZAJI KATIKA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE** umefikiwa na umeingiwa leo tarehe ..14TH.............. ya mwezi wa ..JULY....... Mwaka ..2022......

**BAINA YA BODI YA WADHAMINI YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE (JUHIBU)** ambayo ni Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa (ambao katika mkataba huu watajulikana kama "Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa") ambayo ilianzishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya the Societies Act, Cap. 368 R.E 2002 na Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori, (Cap. 283 R.E. 2009) na Kanuni za Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori, 2018 na imesajiliwa kwa minajili ya kusimamia Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge ya S.L.P 104 Babati, Manyara, Tanzania, kwa upande mmoja.

NA

M/S. EBN HUNTING SAFARIS LIMITED TANZANIA, kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya sanduku la posta 16532, Arusha, Tanzania (Baada ya hapo itasomeka kama Mwekezaji) ambaye hapa itawajumuisha kama itakavyoonekana na itakavyojulikana itawahusisha vile vile warithi na wahusika wowote wa Mwekezaji na ambaye hapa ana nia ya kuwekeza katika eneo hili la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge kwa upande mwingine. Pande zote mbili katika mkataba huu zitajulikana kama "Wahusika"

**KWA KUWA** Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa (Authorized Association) ikifanya kazi kwa niaba ya Jamii katika eneo lake kwa mujibu wa katiba ya Jumuiya hiyo, Jumuiya hiyo ina mamlaka na uwezo wa kukubaliana juu ya matumizi ya ardhi katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge iliyoko Wilaya ya Babati, mkoa wa Manyara.

**KWA KUWA** Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa imepewa na Mkurugenzi wa Wanyamapori haki ya utumiaji wa rasilimali Wanyamapori kwa matumizi ya uvunaji na yasiyo ya uvunaji katika eneo zima la Jumuiya kulingana na gawio la rasilimali ya Wanyamapori (quota) litakayotolewa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kwa kipindi husika kwa ajili ya uvunaji endelevu.

**KWA KUWA** Mwekezaji ameomba Kwa Jumiya ya Jamii iliyoidhinishwa kugawiwa Kitalu cha uwindaji katika eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo kwa mujibu wa mpango wa kanda wa matumizi ya rasilimali (RZMP/GMP) kwa ajili ya kufanya shughuli za uwindaji wa kitalii.

**NA KWA KUWA** Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa na Mwekezaji kwa mujibu wa kifungu cha 31(7) cha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Namba 5 ya mwaka 2009 imeingia katika mkataba kuwezesha mwekezaji kufanya shughuli za uwindaji wa kitalii katika eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo kwa mujibu wa Mpango wa Kanda wa matumizi ya rasilimali (RZMP/GMP).

**SASA INASHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

Kwamba Jumuiya Iliyoidhinishwa na Mwekezaji wameingia na kufikia makubaliano yenye masharti na kwa maelezo yanayoainishwa hapa chini: -

## 1. LENGO LA MKATABA

***1.1 Lengo ambalo mkataba huu umeingiwa ni:***

a) Kukusanya pamoja ujuzi, maarifa, fedha na mali (Assets) ya Jamii husika na Mwekezaji kwa lengo la kuleta maendeleo kwa kutumia rasilimali za Wanyamapori na shughuli nyingine za kiuchumi zinazoandamana na rasilimali hizo katika eneo la Jumuiya.

b) Kutoa ujuzi unaohitajika wa kiufundi, kifedha na kimenejimenti kwa ajili ya mafanikio ya mradi wa uwekezaji.

c) Kuhakikisha kuwa wanajamii wa eneo husika wanapata gawio la haki la manufaa yanayotokana na utumiaji wa mali zilizo chini ya mamlaka yao na pia kuhakikisha kuwa maslahi ya Mwekezaji yanalindwa na kupata kinga ya kudhaminiwa.

## 2. WAJIBU WA WAHUSIKA

**2.1 Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa inakubali hapa kwamba:**

a) Itajitahidi kuhakikisha kuwa eneo lote la uwekezaji chini ya Mkataba huu halina makazi ya binadamu yawe ya muda au vinginevyo kwa muda wote wa mkataba huu.

b) Itampa Mwekezaji au wakala wake haki ya kuingia katika eneo la uwekezaji wakati wowote.

c) Haitatoa haki yoyote ya utumiaji kwa mtu yeyote mwingine kuendesha biashara katika eneo hilo husika ambalo huyo Mwekezaji yupo.

d) Itamwarifu Mwekezaji na kumhusisha katika mambo yote ambayo Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa itaamini kuwa yatakuwa na athari katika kuendelea kuwepo kwa uwekezaji huo au shughuli za Mwekezaji katika eneo la Jumuiya.

e) Haitaingia katika mkataba mwingine wowote au kuungana na chombo chochote kingine ambacho utekelezaji wake utaleta madhara katika shughuli za Mwekezaji bila ya kumuarifu kabla ya kutaka kufanya hivyo na kupata ridhaa ya Mwekezaji.

f) Itaitisha mikutano ya menejimenti kila baada ya miezi sita ambapo kutakuwa na vikao viwili katika mwaka.

g) Endapo kutakuwa na dharura vikao vitafanyika kama itakavyokubaliwa kati ya Mwekezaji na Jumuiya.

h) Jumuiya itaunda Kikosi Kazi (Joint Task Force) kitachoratibu utekelezaji wa Mkataba huu kila baada ya miezi mitatu ambacho kitahusisha wawakilishi kutoka kwenye Jumuiya na Mwekezaji.

i) Jumuiya itahakikisha kuwa Mwekezaji anapata nyaraka zote muhimu katika uendeshaji wa shughuli za uwekezaji.

j) Itawajibika kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakaeingiza mifugo kwenye eneo la uwekezaji.

k) Jumuiya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya itadhibiti uvuvi kwenye eneo la uwekezaji.

**2.2 Mwekezaji anakubali kwamba:**

**A. Masharti ya Jumla**

i. Atatoa fedha yote ambayo inahitajika kwa ajili ya ufanisi wa biashara iliyowekezwa.

ii. Atatoa vifaa na mali zote zinazohitajika kwa ajili ya mafanikio ya uwekezaji huo.

iii. Mali yote isiyoondosheka na mali ya kudumu ambayo kuondolewa kwake kunaweza kuleta madhara kwa mazingira itakuwa mali ya Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa baada ya kumalizika kwa mkataba.

iv. Atajenga na kutunza majengo yote muhimu kwa uwekezaji huo na kabla ya kufanya hivyo atatakiwa kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa jumuiya ya jamii iliyoidhinishwa.



Hlui$ Ar

v. Ataheshimu utamaduni na mila za jamii ya eneo hilo.

vi. Hataihusisha Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa katika athari za kifedha za aina yoyote ile au uwajibikaji unaohusiana na mkataba huu.

vii. Atalitangaza eneo la Jumuiya ndani na nje ya nchi.

viii. Atafundisha na kuajiri wakazi wa eneo husika katika shughuli za kila siku za mradi huo. Mwekezaji atatakiwa kuajiri angalau si chini ya asilimia 60 ya wafanyakazi wake kutoka kwa wakazi wa eneo hilo.

ix. Hataingilia, kuvuruga au kutumia nyenzo za kisiasa, kifedha au kiuchumi kwa namna yoyote ile kwa lengo la kushinikiza shughuli za kila siku za utawala za Jumuiya kwa faida yake.

x. Hatafuga au kuruhusu kufugwa mifugo au wanyama wa nyumbani katika ardhi ya eneo hilo.

xi. Hatatumia ardhi iliyotolewa kwa ajili ya uwekezaji kwa matumizi mengine chini ya Sheria ya Wanyamapori nje ya yale yaliyokubaliwa katika Mkataba bila ya kupata kwanza kibali cha maandishi cha Jumuiya.

xii. Hatapangisha au kuhamisha kwa namna yoyote ile Mkataba huu au sehemu yake bila ya kupata kibali cha maandishi cha Jumuiya kilichopatikana katika mkutano mkuu wa Jumuiya ambacho kimeitishwa kihalali kwa madhumuni ya kujadili na kufikiria ombi la kutoa kibali hicho.

xiii. Mali yote inayohamishika na isiyohamishika inayotumika katika shughuli za uwekezaji huo itakuwa mali ya Mwekezaji katika uhai wa Mkataba huu na kwamba Mwekezaji hataazimisha, kukodisha au kupangisha mali yoyote isiyoondosheka kwa ajili ya kutumia mali hiyo bila ya kupata kibali cha maandishi cha Jumuiya.

xiv. Atashiriki na kusaidia katika doria na ulinzi wa rasilimali katika eneo la Jumuiya ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa mbalimbali kuwezesha zoezi hilo.

xv. Atalipa kiasi cha **USD. 25,000 mara tu** atakapopatiwa kitalu hicho zikiwa ni fedha za kusaidia mfuko wa WMA ambazo zitalipwa kila mwaka.

xvi. Kusaidiana na wananchi katika kuendeleza miradi ya maendeleo katika sekta za afya, elimu, maji, mifugo na barabara, kwa kuilipa Jumuiya kiasi cha **USD. 25,000** kwa ajili ya vijiji 10 kila mwaka kuchangia maendeleo ya vijiji. Fedha hizi zipo nje ya zile zinazotolewa kwa malipo ya uwindaji chini ya kifungu cha 6 cha Mkataba huu.

xvii. Kushirikiana na jumuiya ya jamii iliyoidhinishwa katika kusimamia rasilimali ya Wanyamapori iliyomo ndani ya eneo lake la utawala ili ziweze kuwanufaisha wananchi wake.

xviii. Mwekezaji achangie utoaji wa elimu ya uhifadhi kwa jamii inayomzunguka na WMA kwa ujumla wake.

**B. Masharti ya shughuli za uwindaji wa kitalii**

i. Atatoa huduma za msingi za kijamii kama ilivyokubaliwa katika Mkataba.

ii. Atawaruhusu wana jamii wa eneo hilo, baada ya kupata kibali kutoka kwa Jumuiya, kuingia katika eneo la Jumuiya kwa ajili ya kufanya ibada na matambiko ya kimila ili mradi tu shughuli hizo hazitakuwa na madhara kwa vifaa na shughuli za uwekezaji.

iii. Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa itaajiri kikosi cha doria cha Askari wapatao kumi ambapo mwekezaji atawajibika kulipa **Tshs 90,000,000/=** (Shilingi za Tanzania milioni tisini tu) kwa mwaka fedha zitalipwa katika akaunti ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa. Ili Jumuiya iweze kuwalipa askari hao

iv. Kutoa magari mawili aina ya (land cruiser pickup) mapya ambapo gari moja litatolewa mara tu baada ya kusaini mkataba katika mwaka wa kwanza wa miaka mitano ya mwanzo na gari lingine litatolewa katika mwaka wa kwanza wa miaka mitano ya mwisho gari hizo zitakuwa mali ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa na kusajiliwa kwa Jina la Jumuiya.

v. Kutoa motisha ya **Tsh. 500,000/=** (Shilingi za Tanzania Laki tano tu) kwa kila mwananchi au kikundi kitakachotoa habari za siri (informer) zitakazofanikisha kuwafichua, kukamatwa na kufikishwa mahakamani jangili/majangili wakiwa na nyara zitokanazo na wanyama wafuatao: - Tembo, Twiga, Simba, Chui na Nyati.

vi. Kutoa motisha ya kiasi cha **Tsh. 200,000/=** (Laki mbili tu) kwa mtu yeyote atakayefanikisha kukamatwa bunduki itakayobainika kutumika katika ujangili.



Elias

Ar

**C. Masharti ya shughuli za Utalii wa picha**

i. Kuchangia fedha kiasi cha **USD. 3,000** kwa ajili ya mfuko faraja ambao utahusika na kudhibiti migongano ya wanyamapori na binadamu pamoja na kutoa faraja kwa familia ya mtu/watu aliyekutwa na mauti yaliyosababishwa na wanyamapori. Fedha hizi zitalipwa kila mwaka mwezi Julai.

ii. Mwekezaji atalipa kiasi cha dola za kimarekani kumi (**USD 10)** kwa kila mgeni atakayekuwa anaingia kwenye eneo la **WMA** kwa ajili ya kufanya shughuli za kitalii kwa kila siku.

iii. Fedha hizi zinazotajwa katika kipengele **2.2 C (i)** cha mkataba zitalipwa katika Akaunti ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa ambayo itatolewa katika hati ya madai.

## 3. USIMAMIZI WA MALIASILI

### 3.1 Mwekezaji anakubali kufanya yafuatayo:

a) Kuchukua hatua zote muhimu kuzuia mmomonyoko wa udongo na uharibifu mwingine wa ikolojia ndani ya eneo la Jumuiya kama inavyotakiwa na Sheria.

b) Kutokuondoa, kuuza, kuharibu au kuruhusu kuondolewa kwa mchanga, changarawe, udongo, mawe au mbao kama inavyotakiwa na Sheria.

c) Kutokata miti yoyote bila kibali cha maandishi cha Jumuiya.

## 4, KUGAWA AU KUACHIA UMILIKI

Mwekezaji anaahidi kwamba hatapangisha, hatakabidhi wala kumpa mtu au kutoa kwa mtu yoyote umiliki wa haki yake au kifaa au nyenzo yoyote au sehemu yake ambayo imetolewa kwa ajili ya uwekezaji na Jumuiya chini ya Mkataba huu.

## 5. DHAMANA YA UTEKELEZAJI

Mwekezaji atatoa fedha ya dhamana ya utekelezaji ya **Dola za Kimarekani 20,000/=** (Dola Elfu Ishirini za Kimarekani), ambazo zitawekwa katika akaunti ya pamoja ya Mwekezaji na Jumuiya ya jamii Iliyoidhinishwa ikiwa ni dhamana kuwa atatekeleza yaliyomo katika Mkataba kwa maendeleo ya mradi wa uwekezaji. Kiasi hicho cha fedha pamoja na riba itakayotokana na kiasi hicho zitakamatwa na kuchukuliwa na Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa pale ambapo Mwekezaji

atatelekeza/atatoroka au kuacha mradi huo wa uwekezaji au zitakapohitajika kwa ajili ya kukaza hukumu dhidi ya mwekezaji pale ambapo Mwekezaji ameshindwa kufanya malipo yanayotakiwa. Fedha hiyo ya dhamana ya utekelezaji pamoja na riba yake vitarejeshwa kwa mwekezaji mwisho wa mkataba ukifika. Fedha hii italipwa ndani ya mwezi mmoja baada ya kusainiwa Mkataba huu.

## 6. ADA KWA AJILI YA HAKI YA KUENDESHA SHUGHULI

Ada kwa ajili ya haki ya kuendesha biashara ya safari zitatolewa kwa kufuata viwango vifuatavyo:

6.1 Mwekezaji atalipa kiasi cha **USD. 60,000.00** kwa mwaka kwa Jumuiya kama ada ya Kitalu cha Uwindaji. Aidha mwekezaji atalipa nyongeza ya ada ya kitalu kiasi cha USD 10,000.00 na fedha hizo zitalipwa katika akaunti ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhishwa.

6.2 Ada hii ya Dola za Marekani Elfu sitini **USD 60,000.00** italipwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ambaye atazigawanya kwa mujibu wa mgawanyo wa mapato kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori.

6.3 Mwekezaji atalipa Ada ya Wanyama pamoja na ongezeko la asilimia kumi 10% ya Ada ya kila mnyama atakayewindwa kila mwaka kwa ajili ya kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalii (Tourist Hunting) katika eneo la uwindaji wa kitalii lenye ukubwa wa kilometa za mraba **157.5** (Mia moja hamsini na saba nukta tano tu) ikiwa ni eneo lote lililotengwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii ndani ya eneo la Jumuiya kwa kuzingatia alama za mipaka (beacons) kama ilivyoonyeshwa kwenye Ramani iliyoambatanishwa na kama ilivyooneshwa kwenye Mpango wa Jumla wa Matumizi ya Rasilimali (General Management Plan-GMP) iliyoambatanishwa hapa na kujulikana kama Kiambatanisho **"A"; ili kuondoa utata wa ukubwa wa eneo** la kitalu cha uwindaji, alama za mipaka na alama za kudumu za asili (physical features) zitatumika.

6.4 Ada ya haki ya matumizi kama ilivyotajwa katika aya ya 6.1 hapo juu kwa mwaka **2022** italipwa mara tu baada ya Mkataba huu kusainiwa. Kuanzia mwaka **2023** na kuendelea ada hii italipwa kabla ya tarehe 01 mwezi Januari ya mwaka husika.

6.5 Ongezeko la asilimia kumi (10%) la Ada ya kila Mnyamapori atakayewindwa katika kipengele cha 6.3 litalipwa katika akaunti ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa itakayokua imetolewa katika hati ya madai kila mwezi June wa mwaka wa fedha wa JUHIBU.

## 7 KINGA

Mwekezaji atakata bima kwa jina lake ili kukabiliana na madhara au athari zote zitakazotokana na uharibifu au hasara itakayompata mtu yeyote kutokana na kutumia sehemu na huduma ya utalii au huduma nyigine zinazoambatana na utalii na hivyo kuiwekea kinga Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa kutolipa chochote kutokana na aina yoyote ya athari na madhara. Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa itampa Mwekezaji kinga ya kutodaiwa au kushitakiwa kwa chochote au kudaiwa gharama ya aina yoyote ile kwa mambo yote yaliyofanyika kabla ya Mkataba huu kuingiwa na kuanza kufanya kazi.

## 8 VITULIZO VYA KIMAHAKAMA (RELIEFS), TAFSIRI NA SHERIA YA KUTUMIKA

Kuvunjwa kokote kule kwa Mkataba huu kutampa haki yule aliyeathirika kutafuta vitulizo mahakamani (Reliefs) kwa mujibu wa sheria, kanuni na msingi inayosimamia mikataba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Masuala au maswali yoyote yatakayojitokeza kuhusiana na tafsiri ya maneno au neno lolote au msemo ambao umo katika Mkataba huu utatafsiriwa kwa mujibu wa tafsiri au matumizi yake kulingana na sheria husika za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 9 SHERIA ITAKAYOTUMIKA, USULUHISHI NA UTATUZI WA MIGOGORO

a) Mkataba huu na utekelezaji wake utaongozwa na kutafsiriwa katika hali zote kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Mgogoro wowote au kutokuelewana kunakoweza kutokana na/au unaohusika na/au kushabihiana na utekelezaji wa Mkataba huu utatulizwa kwa maelewano katika mikutano ya mara kwa mara itakayoitishwa na pande zote. Wahusika wa Mkataba huu wanakubaliana kuwa mgogoro au suala lolote la kutokuelewana litapelekwa kwa Msuluhishi kwa mujibu wa Sheria husika. Kabla ya suala lolote kupelekwa kwa Msuluhishi kwa mujibu wa Sheria pande zote

zitahakikisha kuwa njia nyingine za kutatua mgogoro huo zimetumiwa katika kujaribu kupata usuluhishi.

c) Rejeo lolote chini ya kipengele hapo juu litakuwa na maana ya rejeo kwa Msuluhishi katika maana na mujibu na kadri ya matakwa ya vifungu vya **Sheria ya Usuluhishi** (Sura ya 15 ya Sheria za Tanzania Toleo Lililorekebishwa 2002) ama Sheria yoyote itakayotungwa ama marekebisho yoyote ya Sheria yatakayofanywa na Sheria hiyo itakayokuwa inatumika wakati huo.

## 10 UTUNZAJI NA UONAJI WA KUMBUKUMBU

Mwekezaji atatunza na kuweka kumbukumbu na vitabu vya mahesabu na kuvitoa kwa Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa kwa ajili ya ukaguzi vikiombwa. Mwekezaji atatoa vitabu na kumbukumbu hizo kwa ajili ya Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa kujiridhisha juu ya mwenendo wa shughuli ya uwekezaji. Kukataa kutoa kumbukumbu na vitabu hivyo kutaipa Jumuiya haki ya kutumia kifungu cha 9 (b) & (c).

## 11 UENDESHAJI NA MUDA

Ikielezwa hapa vinginevyo au katika Sheria iliyopo ambayo Mkataba huu umefungwa nayo, basi Mkataba huu utachukuliwa kuwa ulianza kutumika siku ambayo ulitiwa saini na wahusika au mtu yeyote mwenye idhini kwa niaba ya upande wowote.

Mkataba huu utatumika kwa kipindi cha miaka kumi (10) na utaanza kutumika kuanzia tarehe 01 Mwezi 01 Mwaka 2023 na utakoma tarehe 31 Mwezi 12 Mwaka 2032 Aidha, muda wa Mkataba huu unaweza kuongezwa kwa kuzingatia kanuni za WMA.

## 11.1 KUANZA KUTEKEZWA KWA MASHARTI YA MKATABA

Pande zote mbili za mkataba huu zinakubaliana kwa pamoja kuwa kwa kusainiwa kwa mkataba huu masharti yote yaliyomo kwenye mkataba huu yatakuwa na nguvu kisheria kwa kipindi cha miaka kumi (10) kuanzia tarehe 01 mwezi 01 mwaka 2023 na kwamba kabla ya tarehe hiyo mkataba huu hautakuwa na nguvu kisheria na kwamba hakuna upande wowote utakaofungwa na mkataba huu kabla ya tarehe,mwezi,mwaka uliokusudiwa.

## 12 MAREKEBISHO

Pande zote zinaweza kwa makubaliano kuufanyia marekebisho Mkataba huu au sehemu yake yoyote kama zikiona kuwa inafaa kufanya hivyo ili kukidhi haja ya mabadiliko ya sheria, sheria ndogo, kanuni, sera au pale inapoonekana kuwa inafaa kufanya hivyo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Mkataba. Pamoja na hivyo, wahusika wanakubaliana kuwa kila baada ya mwaka Mmoja watafanya mapitio ya Mkataba huu kwa kuzingatia mwenendo wa mapato na kufanya maboresho kwa kadiri itakavyofaa. Endapo itabainika kuwa hakuna ongezeko la msingi la mapato makubaliano ya awali ya Mkataba yataendelea.

## 13 KUSITISHWA KWA MKATABA

Mkata huu utasitishwa kwa mujibu wa kanuni za wmA

## 14 FIDIA

Pande zote zinakubaliana hapa kuwa Mkataba huu utakapoisha na ikawa hauongezewi muda basi: -

a) Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa inaweza kumtaka Mwekezaji kuondoa uwekezaji alioufanya ndani ya eneo la uwekezaji na kumtaka kuirejesha ardhi katika hali inayokubalika kwa Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa katika kipindi cha miezi mitatu ya kalenda. Katika kuitumia haki hiyo Jumuiya ya jamii iliyoidhinishwa inatakiwa impe notisi ya miezi sita. Itakapotokea kuwa Mwekezaji ameshindwa kuondoa uwekezaji huo alioufanya basi Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa inaweza kuondoa uwekezaji huo kwa lengo la kurejesha ardhi katika hali yake ya awali na kuchukua fedha kwa kazi hiyo kutoka kwenye akaunti ya pamoja ya dhamana ya utekelezaji.

b) Iwapo itatokea kwamba Mwekezaji hadai maendeleo yoyote yaliyofanywa naye basi mali yote itahamia kwa Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa na hakutakuwepo na ulipaji wa fidia yoyote ile.



Pttais

Ik

## 15 NOTISI/TAARIFA

Notisi au taarifa yoyote au mawasiliano ya kimaandishi yatatumwa au kupelekwa kwa wahusika na kila muhusika atachukuliwa kuwa ametumiwa au amepokea notisi/taarifa ikiwa tu notisi/taarifa hiyo itawasilishwa kwake kwa barua ya rejista.

Mwekezaji ikiwa notisi/taarifa itatumwa kwa;

***M/S. EBN HUNTINGS SAFARIS LIMITED TANZANIA,***
***S.L.P. 16532,***
***ARUSHA.***

Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa ikiwa notisi/taarifa itatumwa kwa;

***KATIBU,***
***JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE,***
***S.L.P. 104, BABATI, MANYARA.***

## 16 GHARAMA

Kila upande husika utajigharamia gharama zake halali na masurufu kuhusiana na Mkataba huu. Mwekezaji atawajibika kulipia gharama za sasa na zitakazozuka baadaye za ushuru wa stampu na usajili kuhusiana na Mkataba huu.

## 17 HAKUNA UTENGUAJI WA HAKI

Kushindwa kutekeleza ama kuchelewa katika utekelezaji wa haki ama nafuu chini ya Kanuni ama Mkataba huu hakumaanishi utenguaji wa haki husika ama nafuu ama kuondosha haki ama nafuu nyinginezo. Hakuna utekelezaji ama sehemu ya utekelezaji wa haki ama nafuu unaoelezewa katika Sheria ama Mkataba huu ama utekelezaji wa haki na nafuu nyinginezo. Haki na nafuu chini ya Mkataba huu ni jumuisho wala hazibagui haki na nafuu zitolewazo na Sheria.

## 18 MAKUBALIANO KWA UJUMLA

a) Mkataba huu na makubaliano yaliyomo ndani yake unawakilisha maelewano ya pande husika na hakuna makubaliano mengine baina ya wahusika kuhusiana na mada ya Mkataba huu, na hakuna mabadiliko ama marekebisho ya Mkataba huu yatakayokuwa na maana ama kuubana upande wowote husika isipokuwa kama;

   i. yamefanywa kwa maandishi,

   ii. yana Hadidu za Rejea kwenye Mkataba huu,

   iii. yametiwa saini na wahusika wa Mkataba huu ama wateule wao,

b) Kwa ajili ya uzingatiaji ama utekelezaji, vipengele vyote vya Mkataba huu vitaendelea kuwa na nguvu zote na ushawishi bila ya kujadili kwamba Mkataba umeisha.

**KWA USHUHUDA HUU BASI**, upande wa Mwekezaji na Upande wa Jumuiya Iliyoidhinishwa katika Mkataba huu wameweka saini zao hapa chini;

**UMETIWA SAINI, MUHURI NA KUTOLEWA** na chapa ya
**JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYMAPORI BURUNGE**

............JUHIBU.................. **MHURI**

*(Jina la ofisi ya AA yenye mamlaka)*

............MWADA..........................

(Jina la mahali/Mji)

Leo tarehe.....14th......... Mwezi wa ..JULY...... Mwaka ..2022...

Jina ..PATRICIA......W. MOSEA............ (Ofisa mwenye mamlaka)

Nafasi katika AA ..M/KITI....WA....BODI.............

Saini.................................................

MWENYEKITI BODI YA WADHAMINI
S.L.P. 104
BABATI-MANYARA
JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE

**Akishuhudiwa na:-**

Jina ..BENVON BUNGE MWAJE...............

Saini.................................................

Wadhifa........KATIBU - JUHIBU..................

Tarehe.........14/07/2022.......................

JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE
KATIBU MKUU
S.L.P 104 - BABATI

**UMETIWA SAINI, MUHURI NA KUTOLEWA** na chapa ya
**EBN HUNTING SAFARIS LIMITED TANZANIA**

............EBN hunting safari.......... **MHURI**

*(Jina la ofisi ya kampuni yenye mamlaka)*

............MWADA.........

(Jina la mahali/Mji)

Leo tarehe.....14th......... Mwezi wa ..July...... Mwaka ..2022..

Jina .......NICOLAS....NEGRE.................... (Ofisa mwenye mamlaka)

Nafasi katika Kampuni ........Director.....................

Saini.................................................

**Akishuhudiwa na:-**

Jina ..Charles Nyangi Sylvester..........

Saini.................................................

Wadhifa.......Company Secretary..............

Tarehe.......14th July, 2022......................

EBN HUNTING SAFARIS
e.b.n
Hunting
P.O.BOX 16532 ARUSHA